# TUPIGE HATUA YA SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA
# MAKALA YA KISWAHILI SEKONDARI MSINGI
# GREDI 7-9

Hezron
BWANA 0712024122

## YALIYOMO

UAKIFISHAJI ........ 2
MANENO YA KISWAHILI NA MIGAWANYO YAKE ........ 5
UYAKINISHI NA UKANUSHO ........ 13
VINYUME/ANTONIMU ........ 14
NYAKATI/NJEO NA HALI ........ 16
SENTENSI YA KISWAHILI ........ 20
NGELI ZA KISWAHILI ........ 21
UMOJA NA WINGI ........ 24
UKUBWA NA UDOGO ........ 26
USEMI HALISI NA USEMI WA TAARIFA ........ 27

## UAKIFISHAJI

**Alama za kuakifisha na matumizi yake.**

| ALAMA | MIFANO |
|---|---|
| **Alama ya Kikomo au Kituo Kikuu(.)** | |
| Kuonyesha mwisho wa sentensi. | |
| Katika kufupisha maneno. Kwa mfano; | *U.N.O, K.B.C, Y.C.S, Dkt. Maktaba, Bw. Msumari* |
| Kuonyesha Saa. Kwa mfano; | *Misa ilianza saa 4.30 za asubuhi.*<br>*Hivi sasa ni saa 10.20.* |
| Katika hesabu kuonyesha sehemu isiyo nzima. Kwa mfano; | *Ukigawa tatu mara mbili, utapata 1.5.*<br>*Mtoto huyo ana uzani wa kilo 8.27* |
| Kuonyesha senti katika pesa. | *Bei yake ni shilingi 12.50.*<br>*Karo ya shule mwaka huu ni 80,000.00* |
| **Alama ya Kituo, Kipumuo au Koma (,)** | |
| Kuorodhesha vitu zaidi ya mbili. | *Nimenunua simu, saa, redio na viatu.*<br>*Kina mama waliimba, wakapiga ngoma na kunegua viuno vyao.* |
| Kugawanya mawazo katika sentensi. | *Baada ya sala za jioni, Mzee Makosa alitoka nje na kuwasha sigara yake.*<br>*Nilipomwuliza kama alimjua binti yule, aliniangalia tu na kucheka*<br>*Ingawa kitabu hiki ni kizito, sina budi kukibeba.* |
| Kutoa maelezo zaidi. | *Shabiba, mmojawapo ya wanawake wajawazito, amejifungua mtoto wa kike.*<br>*Shati hili, ingawa nalichukia, nitalivalia tu.* |
| Katika tarakimu, kugawa elfu. | *Shilingi 209, 408, 000 ziliporwa na serikali.*<br>*Dawa hiyo iliua takribani mbu 61, 247.* |
| **Alama ya Kinukuu (“”)** | |
| Kunukuu usemi halisi | *"Ukitaka kufua dafu," mama akamwambia mwanawe, "lazima utie bidii."*<br>*Alimtazama kisha akamwuliza, "Unadhani nimechanganyikiwa kama wewe?"* |
| Kunukuu kichwa cha kazi ya sanaa k.v kitabu, wimbo, kipindi n.k | *Saumu na Neema ni wahusika katika riwaya "Hamu ya Sumu Tamu".* |

| | |
|---|---|
| | *Rose Muhando ndiye aliyeimba "Mteule Uwe Macho".* |
| Kuonyesha maneno yasiyo ya Kiswahili unapochanganya ndimi katika sentensi | *Huyu ndiye mchezaji "number one."*<br>*Amesema "keyboard" ya "computer" yake haifanyi kazi.* |
| Kuonyesha maneno yanayowakilisha maana tofauti na maana yake ya kawaida au kinaya. | *Lesi alipoenda kwenye 'maktaba' alipata mimba.*<br>*Rais wetu 'mtukufu' amewatisha mawaziri wake.*<br>*Moto ulioteketeza shule hiyo ulitokana na kusudi la wanafunzi la 'kumshtua' mwalimu wao.* |
| Kuonyesha herufi iliyoachwa nje au kufupisha maneno katika ushairi hasa kwa kusudi la kutosheleza idadi ya mizani. | *'takufuata popote wendapo.*<br>*'liapo ya mgambo, lazima kuna jambo.* |
| Katika maendelezo ya sauti ya ung'on'g'o (ng') | *Ng'ombe wa Ng'ang'a wanang'ang'ania nini?*<br>*King'ang'i anapenda kunung'unika ovyo ovyo.* |
| **Alama ya Kiulizi (?)** | |
| Kuulizia swali. | *Je, utamtembelea lini?*<br>*Ariana anaishi wapi?* |
| Kuonyesha pengo lililoachwa wazi. | *Ndama ni mwana wa ng'ombe ilhali ___?___ni mtoto wa mbuzi.*<br>*__?__ mpokee mke wako, __?__, siku ya leo umepata jiko.* |
| **Alama ya Hisi (!)** | |
| Kuonyesha hisia kama vile hasira, mshangao, furaha n.k | *Lo! Ukistaajabu ya Musa utaona ya Firauni.*<br>*Pepo nyeusi! Shindwa! Chomeka! Kwenda kuzimu!* |
| Kuigiza Tanakali za Sauti. | *Amejikwaa sasa ameanguka pu!*<br>*Moyo ulidunda ndu! ndu!* |
| **Alama ya Nukta-Mbili au Koloni (:)** | |
| Kutanguliza orodha. | *Harusi hiyo ilihudhuriwa na watu wa wengi: wake kwa waume; wadogo kwa wakubwa; wazee kwa vijana. Kuna aina kadhaa za vivumishi: vivumishi vya sifa, vivumishi vya idadi, vivumishi viwakilishi na kadhalika* |
| Kuelezea sababu au kuonyesha matokeo ya kitu. | *Saumu alipoingia chumbani alipigwa na butwaa: mamake alikuwa amekufa.*<br>*Baba alinipatia zawadi nzuri sana: nilirukaruka kwa furaha.* |
| Kuonyesha saa. | *Wimbo huo unachukua dakika 4:45.*<br>*Aliingia saa 5:15* |
| Kunukuu ukurasa wa kitabu cha dini. Kama vile Kurani na Bibilia. | *Padre alisoma Luka 2:1-6*<br>*Katika Kurani 1: 2-284-286, Allah anasema...* |
| Kuonyesha maneno ya msemaji katika tamthilia au mchezo wa kuigiza. | *Mzee Mwanyati: Unafikiria mimi ni nyanyako?*<br>*Kadogo: (akitetemeka) Tafadhali naomba unisamehe.* |
| Kuonyesha mada katika barua au. | *KUH: Ombi Lako la Kujiuzulu.*<br>*RE: Barua ya tarehe 3/2/1999.* |
| Katika kumbukumbu za mkutano. | *KUM 2/321/2000: Mbinu mpya za kunyamazisha raia. Ajenda 2: Kusomwa kwa kumbukumbu za mkutano uliotangulia.* |
| **Alama ya Nukta-Kituo au Semi Koloni (;)** | |
| Kuorodhesha vitu hasa vinapokuwa na zaidi ya neno moja. | *Harusi hiyo ilihudhuriwa na watu wa wengi: wake kwa waume; wadogo kwa wakubwa; wazee kwa vijana. Wakati wa likizo* |

| | |
|---|---|
| | *tulitembelea sehemu kadhaa: Mombasa, Kenya; Dodoma,Tanzania; Kampala, Uganda na tukamalizia hapa Nairobi, Kenya.* |
| Kuunganisha vishazi huru viwili au kuonyesha mawazo mawili. | *Tuliwasili darasani tukiwa tumechelewa; mwalimu alitukaribisha kwa kiboko.*<br>*Usiwe na wasiwasi; nitakuwa pamoja nawe siku zote.* |
| **Alama ya Kistari Kifupi (-)** | |
| Kuunganisha maneno mawili. | *Mbwa-koko aliuma mwana-haramu.*<br>*Nawatuma kama wana-kondoo miongoni mwa mbwa-mwitu.* |
| Kuonyesha hadi, au mpaka. | *Bei imepanda kutoka shilingi 20 – 30.*<br>*Tutasoma kitabu cha Matendo 2: 3 - 7* |
| Kama alama ya kupunguza au kutoa katika Hesabu. | *9 - 7 = 2*<br>*4 - 5 = -1* |
| Kuonyesha neno ambalo halijakamilika litaendelezwa katika msitari ufuatao. | *Ukitaka twende kwetu nyumbani <u>nitakupe-leka</u> ukamwone mama yangu ambaye amekuwa mgonjwa kwa muda sasa.*<br>*Alisema kuwa kuna migumo kumi na mitatu katika bustani la Kuzimu amkako <u>kunaami-niwa</u> watu wengi wamefilia huko* |
| Kuonyesha tarehe. | *Watu wengi walikufa tarehe 07-08-1998.*<br>*Marehemu alikufa tarehe 06-06-2006* |
| **Alama ya Kistari Kirefu (–)** | |
| Kutoa maelezo zaidi. | *Nilipokutana na Zakido – ambaye aliripotiwa kupotea miaka miwili iliyopita–nilimsalimia lakini hakunitambua.*<br>*Hatimaye nimeshinda – baada ya kujaribu kwa masaa matatu.* |
| Kuorodhesha hoja au vitu. | *Umuhumu wa fasihi simulizi:*<br>*– kuburudisha*<br>*– kuelimisha*<br>*– kuunganisha jamii* |
| **Alama ya Mabano au Parandesi ()** | |
| Kutoa maelezo zaidi. | *Z. Anto (aliyeimba Binti Kiziwi) ametoa wimbo mpya. Shangazi yangu (ambaye ni naibu wa waziri) amenitumia zawadi.* |
| Kutoa neno jingine lenye maana sawa. | *Dhamira (nia) ya mshairi huyu ni kutushauri tusikimbilie maisha.*<br>*Mabanati (wasichana) hao hutembea uchi jijini usiku wa manane.* |
| **Alama ya Kinyota (*)** | |
| Kuonyesha neno ambalo litaelezewa zaidi chini ya ukrasa(foot note). | *Alipopata nafasi ya kuingia shule ya upili ya Starehe*, mwanafunzi huyo alijawa na furaha tele.*<br>**Starehe ni mojawapo ya shule zinazofanya vizuri zaidi barani Afrika.* |
| Kuficha herufi/silabi katika neno ili kupunguza ukali wa maneno yasiyo na nidhamu. | *Rais aliwaita wananchi m**i ya kuku.*<br>*Aidha, alisema kwamba nyote ni wapu***vu.* |
| **Alama ya Mlazo (/)** | |

| | |
|---|---|
| Kuonyesha 'au' | *Mkutano huo utahutubiwa na Rais/Waziri Mkuu. Wazungumzaji wengi wa Kiswahili wanatoka Kenyz/Tanzania.* |
| Kuonyesha neno au fungu la maneno lenye maana sawa. | *Sheila amepewa cheo cha katibu/mwandishi. Hawa ndio wanaotapatapa ovyo/wasio na mbele wala nyuma.* |
| Katika hesabu kuonyesha kugawanya au akisami. | *5/7 ya siku za juma ni siku za kazi.*<br>*12 / 6 = 2* |
| Katika tarehe. | *Shule zilifunguliwa tarehe 08/01/2012*<br>*Kamati hiyo ilikubaliana kwamba, Mwokozi alizaliwa tarehe 25/12* |
| **Alama ya HERUFI KUBWA** | |
| Kuanzisha sentensi' | *Fisi hula mizoga.*<br>*Huu ndio mwanzo wa sentensi hii.* |
| Kuonyesha Nomino za Kipekee. | *Bi Rangile anatoka Vikwazoni.*<br>*Nchi ya Tanzania imebarikiwa na Mlima Kilimanjaro unaowavutia wageni kutoka Ulaya.* |
| Kuonyesha Kichwa au Mada. | *ALAMA ZA UAKIFISHAJI*<br>*UFAHAMU*<br>*Njia Tano za Kuua Mbu* |
| Kuonyesha maneno yaliyofupishwa. | *UKIMWI ni Ukosefu wa Kinga Mwilini.*<br>*TUKI ni Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.* |

## MANENO YA KISWAHILI NA MIGAWANYO YAKE

**AINA ZA MANENO (Parts of Speech)**

1. **Neno**

Neno huwa ni silabi au mkusanyiko wa silabi zinazotamkwa au kuandikwa ili kuleta maana fulani.

Katika lugha ya Kiswahili kuna aina nane kuu za maneno kama zifuatazo:

1. Nomino (N)- Nouns
2. Viwakilishi (W)- Pronouns
3. Vivumishi (V)-Adjectives
4. Vitenzi (T)- Verbs
5. Vielezi (E)- Adverbs
6. Viunganishi (U)- Conjunctions
7. Vihusishi (H)- Prepositions
8. Vihisishi (I)- Interjections

**NOMINO (N) (Nouns)**

Nomino ni maneno ambayo ni majinaya watu, vitu, hali n.k. Kuna nomino za kawaida na nomino za kipekee miongoni mwa aina nyingine za nomino

**Aina za Nomino**

Kunazo aina mbalimbali za nomino katika lugha ya Kiswahili.

i. **Nomino za Kawaida (Common nouns)**

Haya ni majina ya kawaida yanayoweza kutumiwa kurejelea vitu mbalimbali, watu, wanyama, mahali na kadhalika. Nomino hizi zinaweza kuwa katika umoja au wingi kulingana na ngeli yake.k.m: *nyumba, mbuzi, daktari, soko, kalamu, jua, uji, maji, siku,malazi, mwalimu, ndege, shirika n.k.*

Nomino hizi hazianzi kwa herufi kubwa ila tu zikiwa mwanzoni mwa sentensi.

ii. **Nomino za Kipekee (Proper nouns)**

Hizi ni :

**majina maalum ya watu**: mfano; Juma, Halima, Esther, Onyango.

**Miji**. Mfano; Nairobi, Mombasa, Mogadishu, Paris nk.
**Kampuni**. Mfano;Bidico, Jumia nk.
**Nchi.** Mfano; Tanzania, Uchina, Nigeria nk.
**Raia:** Wakenya, Waganda, Wasomali, Wajerumani, nk.
**Mungu:** mfano; Mola, Rabuka, Rabana, nk.
**Bahari:** mfano; Hindi, Atlantiki na Bahari ya Shamu, nk.
**Maziwa:** mfano; Viktoria, Bogoria, Naivasha, nk.
**Mito.** Mfano; Mto Tana, Mto Zambezi nk.
**Maziwa.** Mfano; Ziwa Victoria, Ziwa Nakuru nk.
**Miezi:** mfano; Machi, Oktoba, Septemba, nk.
**Siku za wiki:** mfano; Jumatatu, Alhamisi, Ijumaa, nk.
**Milima.** Mfano; Mlima Kenya, Mlima Evaresti, Mlima Kilimanjaro nk.
**Sayari:** mfano; Zebaki, Zuhura, Dunia, Mirihi, Mshtarii, Zohali, Sarteni, Kausi na Utaridi.
**Dini:** mfano; Kiislamu, Kikristo, Kihindi, Kimithra, nk.
**Madhehebu:** mfano; Katoliki, Othodoksi, Uprotestanti, nk.
**Makabila:** mfano; Mjaluo, Mtaita, Msomali, Mnandi, nk.
**Lugha:** mfano; kiluhya, Kidegodia, Kisomali, nk.
**Stakabadhi/Miswada/Maafikiano:** mfano; Azimio la Arusha(Arusha Declaration)
**Majina ya viama:** mfano: Chama Cha Mapinduzi (CCM)
**Tanbihi:** Nomino za pekee huanza kwa herufi kubwa, zikiwa mwanzoni, katikati au hata mwishoni mwa sentensi.
Nomino za kipekee haziwezi kubadilika, na hivyo basi hazina wingi.

iii. **<u>Nomino za Jamii/makundi (Collective nouns)</u>**

Nomino za jamii hurejelea kundi la vitu au wanyama, kwa ujumla. Aghalabu vitu vinavyorejelewa hutokea kwa makundi ya vitu mbili au zaidi. Nomino hizi hutumia wingi tu tunaporejelea makundi zaidi ya moja. k.m: *jozi la viatu, umati wa watu, bustani la maua, bunga la wanyama*

iv. **<u>Nomino za Wingi (Non-count nouns)</u>**

Nomino hizi hurejelea vitu ambavyo hutokea kwa wingi na haziwezi kuhesabiwa. Vitu kama hivyo hutumia aina nyingine ya vipimo ili kurejelea kiasi chake. Nomino za wingi hazina umoja. k.m: *maji, maziwa, changarawe, pesa, nywele*

v. **<u>Nomino za Vitenzi Jina (Derivational nouns- nouns derived from verbs)</u>**

Nomino hizi huundwa kutokana na vitenzi kwa kuongeza kiungo KU mwanzoni mwa mzizi wa kitenzi. k.m: *kulima, kuongoza, kucheza, kulala*

vi. **<u>Nomino za Dhahania (Abstract nouns)</u>**

Haya ni majina ya hali au vitu ambavyo havionekani wale haviwezi kushikika. k.m: *upendo, furaha, imani, elimu, ndoto, mawazo, maisha, usingizi*

vii. **<u>Nomino ambatano/ambata</u>**

Nomino mbili zinazounda nomino moja. Huundwa kwa kutumia kistari kifupi ya nomino hizi au kama neno moja kuonyesha kitumizi. Kwa mfano; Isimu-jamii/isimujamii, mwana-chama/mwanachama**,** Elimu-viumbe/elimuviumbe, bata-mzinga/batamzinga**, m**weka-hazina/mwekahazina, kipaza-sauti/kipazasauti

viii. **<u>Nomino milikishi</u>**

Huonyesha uhusiano/umiliki kwa kuhusisha nominoya kawaida na kivumishi kimilikishi. Kwa mfano;

| **Nomino za kawaida** | **Kivumishi kimilikishi** | **Nomino milikishi** |
|---|---|---|
| mtu | wake | mtuwe |
| wimbi | lake | wimbile |
| mkono | wake | mkonowe |
| kaka | yangu | kakangu |
| ngoko | yake | ngokoye |

**<u>VIWAKILISHI (W)</u> (Pronouns**)

Viwakilishi vya Nomino ni maneno yanayotumika badala ya nomino. Kiwakilishi hakiwezi kuambatanishwa na nomino inayorejelewa.

**Aina za Viwakilishi**

i. **<u>Viwakilishi vya Nafsi</u>**

Viwakilishi hivi hutumika kwa niaba ya nafsi kwa umoja na kwa wingi.

Viwalkilishi hivi vimegawika katika sehemu mbili. ***<u>Viwakilishi vya nafsi huru</u>*** na ***<u>viwakilishi vya nafsi tegemezi</u>***.

a) ***Viwakilishi vya nafsi huru***

Hivi ni viwakilishi vya nafsi ambavyo ni maneno kamili, navyo ni; ***mimi, wewe, yeye, sisi, nyinyi, wao***

| **NAFSI** | **UMOJA** | **WINGI** |
|---|---|---|
| Nafsi ya Kwanza | Mimi | Sisi |
| Nafsi ya Pili | Wewe | Ninyi/Nyinyi |
| Nafsi ya Tatu | Yeye | Wao |

**Sisi** tuliwatangulia **nyinyi** kufika hapa.

**Mimi** si mjinga kama vile **yeye** anavyofikiria

b) ***Viwalkilishi vya nafsi tegemezi***

Hivi huwa vile viambishi vinanavyo wakilisha viwakilishi vya nafsi huru.

Zingatia jedwali lifuatalo:

| **Nafsi huru** | | **Viwakilishi vya nafsi huru** | **Mfano katika sentensi** |
|---|---|---|---|
| Nafsi ya kwanza | Mimi | **ni** | 1. **Ni**nasoma.<br>2. **Ni**liona.<br>3. **Ni**takuita.<br>4. **Ni**mesikiza. |
| | Sisi | **tu** | 1. **Tu**nasoma.<br>2. **Tu**liona.<br>3. **Tu**takuita.<br>4. **Tu**mesikiza. |
| Nafsi ya pili | Wewe | **u** | 1. **U**napenda.<br>2. **U**libeba.<br>3. **U**taoga.<br>4. **U**meosha. |
| | Nyinyi | **m** | 1. **M**napendana.<br>2. **M**libebana.<br>3. **M**taoga.<br>4. **M**meosha. |
| Nafsi ya tatu | Yeye | **a** | 1. **A**nacheza.<br>2. **A**lisafiri.<br>3. **A**taburudika. |
| | Wao | **wa** | 1. **Wa**nacheza.<br>2. **Wa**lisafiri.<br>3. **Wa**taburudika. |

ii. **<u>Viwakilishi Viashiria</u>**

Viwakilishi viashiria (vionyeshi) hutumika badala ya nomino kwa kutumia kuonyesha nomino inayorejelewa bila kuitaja. k.m: *huyu, yule, hapa, n.k*

**Hiki** hakina maandishi yoyote.

**Hao** hawajui tofauti ya viwakilishi na vivumishi.

Tumekuja **hapa** ili kuwaburudisha kwa nyimbo tamu tamu.

iii. **<u>Viwakilishi Visisitizi</u>**

Husisitiza nomino inayowakilishwa kwa kuashiria umbali uliopo na kwa kutegemea nafsi. k.m: *yuyu huyu, wawa hawa, kiki hiki, papo hapo, mumu humu,*

**Zizi hizi** ndizo zilizovunjika wiki jana.

**Yuyo huyo** aliyekamatwa juzi, ameiba tena.

**iv. Viwakilishi viradidi**

Husisitiza nomino inayowakilishwa kwa kurudiarudia kiashiria chake. K.m: huyu huyu, hiki hiki, wale wale nk.

Mototo **yule yule** husumbua mno.

Uzi **huu huu** umekatika.

**v. Viwakilishi vya Sifa**

Husimama badala ya nomino kwa kurejelea sifa yake. k.m: '-eupe, -zuri, -tamu, -embamba, -rembo, safi'

**Vyekundu** vimehamisha.

**Warembo** wamewasili.

**Kitamu** kitaliwa kwanza.

**vi. Viwakilishi vya Idadi**

Hutumika kusimama badala ya nomino kwa kurejelea idadi yake.

***a) Idadi Kamili***

Hutumia nambari kuelezea idadi ya nomino. k.m: 'saba, mmoja, ishirini'

**Wawili** wamepigwa risasi polisi leo jioni.

Alimpatia mtoto wake **hamsini** kununua chakula

*b)* ***Idadi Isiyodhihirika***

Huelezea kiasi cha nomino kwa ujumla, bila kutaja idadi kamili k.m: 'chache, nyingi, kadhaa, kidogo, wastani

Tutazungumza na **wachache** k  abla ya kuanzisha maonyesho yetu.

**Kadhaa** zimeripotiwa kupotea.

**vii. Viwakilishi vya pekee**.

Kwa mfano:

***Yeyote*** atachaguliwa kufanya kazi hiyo.

***Chote*** kitaliwa na wagonjwa.

***Lenye*** limenunuliwa limeoza.

***Zenyewe*** zimeraruka vibaya.

***Kwingine*** kutafagiliwa.

***Wengineo*** watajitokeza wakati ukifika.

**viii. Viwakilishi Viulizi**

Viwakilishi viulizi hutumika kwa niaba ya nomino katika kuulizia swali. Baadhi ya viwakilishi viulizi huchukua viambishi vya ngeli. k.m: ' -ngapi?, -pi?'

**Vingapi** vinahitajika? - kuulizia idadi.

**Zipi** zimepotea?

Kunavyo viwakilishi viulizi vingine ambavyo havichukui viambishi vyovyote. k.m: 'wapi?, gani?, nini?, vipi?'

**Gani** imefunga bao hilo?

**Wapi** hapana majimaji?

Yule mvulana alikupatia **nini**?

Uliongea naye **vipi**? - kuulizia namna

**ix. Viwakilishi Vimilikishi**

Viwakilishi hivi hurejelea nomino kwa kutumia vimilikishi. k.m: '-angu, -ako, -ake, -etu, -enu, -ao'

**Kwetu** hakuna stima.

**Lake** limekucha.

**Zao** zimeharibika tena

**x. Viwakilishi Virejeshi**

Hutumia O-rejeshi kurejelea na kusimamia nomino. k.m: 'ambaye, ambao, ambalo, ambacho, huyo, yule'

**Ambalo** lilipotea limepatikana.

**Ambaye** hana mwana, aeleke jiwe

**xi. Viwakilishi Vya A-Unganifu**

Huwakilishi nomino kwa kutaja kinachomiliki nomino hiyo. Huundwa kwa kuambatanisha kiambishi cha nafsi/ngeli pamoja na kiambishi -a cha a-unganifu, kisha nomino nyingine k.m: 'cha, la, kwa, za, ya'
**Cha** mlevi huliwa na mgema.
**Za** watoto zitahifadhiwa.

**VIVUMISHI (V)** (**Adjectives**)
**Vivumishi** au **visifa** ni maneno **yanayotuelezea zaidi** kuhusu **nomino** au **kiwakilishi**. Aghalabu vivumishi hutanguliwa na nomino au kiwakilish.

**Aina za Vivumishi**

**i. Vivumishi vya Sifa**

Hivi ni vivumishi ambavyo hutoa sifa ya kitu, mtu, mahali, n. Kwa mfano: *kizuri, kali, safi, mrembo*
Yule mama **mweusi** hupika chakula kitamu.
Mvulana **mkorofi** aliadhibiwa na mwalimu kutokana na tabia zake mbaya.
Sauti **nzuri** humtoa nyoka **mkali** pangoni

**ii. Vivumishi Vimili kishi**

Vivumishi hivi hutumika kuonyesha nomino inamiliki nyingine. Mizizi ya vivumishi hivi huundwa kulingana na nafsi mbalimbali ( -angu, -ako, -ake, -etu, -enu, -ao). Kwa mfano: *changu, lako, yake, kwetu, vyenu, zao*
Nitatumia talanta **zangu** kwa manufaa ya taifa **letu**.
Aliweka kitabu **chako** sebuleni **mwako.**
Katosha amepata nguo **yake** miongoni katika sanduku **lao**.

**iii. Vivumishi vya Idadi**

Hutueleza zaidi kuhusu kiasi, au idadi ya nomino. Kuna aina mbili za vivumishi vya idadi.

***a) Idadi Kamili***

Hutumia nambari kuelezea idadi ya nomino. k.m: *tatu, mbili, kumi, mia moja na sita nk.*
Msichana **mmoja** amewauwa nyoka **wawili.**
Siku **kumi** zimepita tangu Bi Safina alipojifungua watoto **watatu.**

***b) Idadi Isiyodhihirika***

Huelezea kiasi cha nomino kwa ujumla, bila kutaja idadi kamili k.m: *chache, nyingi, kadhaa, kidogo, wastani*
Watu **wachache** waliohudhuria mazishi ya Kajuta walikula chakula **kingi** sana.
Baba yao alikuwa mateka kwa miaka **kadhaa**.

**iv. Vivumishi Visisitizi**

Husisitiza nomino fulani kwa kurudia rudia kivumishi kiashiria. Kwa mfano: *yuyu huyu, wawa hawa, kiki hiki, papo hapo, mumu humu,*
Jahazi **lili hili.**
Wembe **ule ule.**
Ng'ombe **wawa hawa.**

**v. Vivumishi Viashiria / Vionyeshi**

Vivumishi viashiria hutumika kuonyesha au kuashiria nomino kulingana na **"umbali"**. **Karibu-** hapa, huyu, hiki, hili, huku, haya, ule, wale, pale. **Mbali kidogo-** hapo, huyo, hiyo, hicho. **Mbali zaidi-** pale, lile, kile
Msichana **huyu** ni mkubwa kuliko **Yule.**
Jani **hili** la mwembe limekauka.
Tupa mpira **huo.**

**vi. Vivumishi vionyeshi viradidi**

Hivi hutumika kuonyesha au kuashiria nomino kulingana na umbali lakini kwa kujirudia na kutilia mkazo. Kwa mfano:
Mwanafunzi **huyu huyu** alikimbia mbio ajabu.
Kitabu **hiki hiki** kilipatikana maktabani

**vii. Vivumishi Viulizi**

Vivumishi viulizi hutumika kuuliza swali. Baadhi ya vivumishi viulizi huchukua viambishi vya ngeli. Kwa mfano: *-ngapi?, -pi?*
Ni walimu **wangapi** wamefukuzwa? - kuulizia idadi.
Je, ni dawati **lipi** lenye funguo zangu?
Kunavyo vivumishi viulizi vingine ambavyo havichukui viambishi vyovyote. k.m: *wapi?, gani?, nini?, vipi?*
Unazungumza kuhusu kipindi **gani**?
Je, mmefika mahali **wapi**? - kuulizia mahali

**viii. Vivumishi Virejeshi**

Hivi ni vivumishi ambavyo hurejelea nomino. Vivumishi hivi vinaweza kuwa vivumishi vya O-rejeshi au vivumishi viashiria vinapotumika kurejelea nomino. k.m: *ambaye, ambao, ambalo, ambacho*
Msichana **ambaye** alikuja ni Sheila.
Sauti **ambayo** uliisikia ilikuwa ya Mzee Kasorogan

**ix. Vivumishi vya KI-Mfanano**

Vivumishi vya KI- ya Mfanano hutumika kulinganisha sifa ya nomino na hali au tabia nyingine. Vivumishi hivi hutanguliwa na nomino, kisha kiunganishi/kihusishi cha A-unganifu kisha neon linalofuata huchukua kiungo KI. Kwa mfano: *wa kifalme, za kijeshi, ya kitajiri, n.k*
Chifu wa **Vikwazoni** anaishi maisha ya **kimasikini.**
Chali anapenda kusikiliza mziki wa **kizungu.**
Bi Naliza huvulia mavazi ya **kifalme**.

**x. Vivumishi Vya A-Unganifu**

Vivumishi hivi hutuelezea zaidi kuhusu nomino kwa kuonyesha kitu kinachomiliki nomino hiyo. Huundwa kwa kuambatanisha kiambishi cha nafsi/ngeli pamoja na kiambishi **"-a"** cha a-unganifu, kisha nomino. Kwa mfano: *cha, la, kwa, za, ya*
Watoto **wa** mwalimu mkuu wana tabia nzuri.
Chai **ya** daktari imemwagika.

**xi. Vivumishi vya pekee.**

Kwa mfano:

Mtu ***yeyote*** atachaguliwa kufanya kazi hiyo.

Chakula ***chote*** kitaliwa na wagonjwa.

Embe ***lenye*** limenunuliwa limeoza.

Nguo ***zenyewe*** zimeraruka vibaya.

Mahali ***kwingine*** kutafagiliwa.

Wanawake ***wengineo*** watajitokeza wakati ukifika.

**Tanbihi:** Ieleweke kuwa **vivumishi vya a-unganifu** havipo tena**,** bali a-unganifu ikija baada ya **nomino** au baada ya **kiwakilishi** itakuwa **kihusishi.**

**VITENZI (T)** (**Verbs**)

Vitenz ni maneno yanayosimamia kitendo. Kila kitenzi huwa na shina la kitenzi (sehemu ndogo zaidi ya kitenzi ambayo ndiyo huwakilisha tendo hilo). Shina la kitenzi huambatanishwa na viambishi ili kutoa maana iliyokusudiwa kama vile mtendaji, mtendewa, wakati kitendo kinafanyika na pia kauli ya kitenzi hicho.

**Aina za Vitenzi**

**i. Vitenzi Halisi**

Hivi ni vitenzi ambavyo huchukua viambishi mbalimbali, kama vile; viambishi vya nafsi, ngeli, wakati, virejeshi, mtenda/mtendwa, mnyambuliko na kadhalika.

Vitenzi hivi hutokea kama kitenzi kimoja tu katika sentensi.

Hivi ni vitenzi vinavyorejelea vitendo vya kutendeka au kutotendeka. k.m: *soma, kula, sikiza*
Waziri Mwasimba aliwasili jana kutoka ng'ambo.
Kawia atapikia wageni.

Funga mlango wa dirisha.

ii. **Vitenzi vikuu**

Vitenzi hivi huchukua muundo sawa na vitenzi halisi Ila tofauti ni kuwa vitenzi hivi huitwa vitenzi vikuu pale kumetokea na vitenzi viwili au zaidi katika sentensi moja.

Kwa mfano;

I. Aliumia alipokuwa **anacheza**.
II. Mwanafunzi alitarajiwa **afuzu** mtihani huo.
III. Atokapo huwa **amefunga** kilemba.

**iii. Vitenzi Visaidizi (Helping/Auxiliary verbs)**

Vitenzi hivi huandamana na vitenzi vikuu ili kutoa maana kamili iliyokusudiwa katika sentensi.

Vitenzi visaidizi aghalabu hutangulia vitenzi vikuu katika sentensi.

Vitenzi visaidizi hutangulia vitenzi halisi (vitenzi vikuu) katika sentensi ili kuleta maana inayokusudiwa kulingana na wakati au hali. k.m: *-kuwa, -ngali,*

Jua **lilikuwa** limewaka sana.
Bi Safina **angali** analala
Wabunge **wanataka** kulipwa mishahara mikibwa.
**Walikuwa** **wanataka** wamtembelee mgonjwa.
**Nlikuwa** **naenda** kuandika somo la Historia.

**iv. Vitenzi sambamba**

Vitenzi sambamba huwa vitenzi viwili au zaidi vinavyotumika pamoja ili kutoa dhana moja yenye maana kamili.

Aina hii ya vitenzi huundwa kwa vitenzi visaidizi na vitenzi vikuu

Vitenzi sambamba vinapotokea katika mfululizo, vyote hutumia kiambishi awali cha kiwakilishi nafsi kile kile kimoja.

Kwa mfano:

I. **Alikuwa angali anataka kuendesha** gari.
II. a**ngeenda angekuwa amekwisha Kula.**
III. **Waliwakuta wakiwa wangali wanalalamika.**

**v. Vitenzi Vishirikishi**

Vitenzi vishirikishi hutumika kuelezea hali iliyopo au mazingira. Vitenzi hivi huonyesha uhusiano kati ya **kiima** na sehemu nyingine ya sentensi.

Hivi vimegawika katika sehemu mbili: ***vitenzi vishirikishi vikamilifu*** na ***vitenzi vishirikishi vipungufu.***

***a) Vitenzi vishirikishi vikamilifu***

Hivi ni vitenzi vinavyoweza kuchukua viambishi vya ngeli, nafsi na wakati.

Kwa mfano:

i) Msafiri **angali** safarini.
ii) Mama **hajawa** mzima kwa kipindi cha juma nzima.

**Tanbihi:**

**1.** Vitenzi vishirikishi vikamilifu vinaweza kuchukua muundo sawa na vitenzi visaidizi. Tofauti hubainika tu katika muktadha wa sentensi. Vitenzi vishirikishi vikamilifu hutokea pekee katika sentensi ilhali vitenzi visaidizi sharti viandamane na vitenzi vikuu katika sentensi. Kwa mfano:
   a. Ng'ombe **alikuwa** zizini. (Kitenzi kishirikishi kikamilifu)
   b. Ng'ombe **alikuwa** amefungwa zizini. ( Kitenzi kisaidizi)
   c. Mwalimu mkuu **hajawa** shuleni. (Kitenzi kishirikishi kikamilifu)
   d. Mwalimu mkuu **hajawa** akija shuleni. (Kitenzi kisaidizi)

**2.** Ingawa vitenzi vishirikishi vikamilifu hutokea pekee katika sentensi na huchukua viambishi vya nafsi, ngeli na wakati, mwanafunzi asije akavichanganya na vitenzi halisi. Kwani vitenzi vishirikishi vikamilifu **haviwezi vikanyambulika abadani.**

*b) Vitenzi vishirikishi vipungufu*

Hivi ni vile vitenzi visivyoweza kuchukua viambishi vya wakati, hivyo kupungukiwa kwa kiasi fulani. Mfano wa vitenzi hivi ni kama; **si, ni, yu, li, Zi, wa, ndi, ki, vi** n.k.

a. Mwalimu wetu **ni** mkarimu.
b. Mungu **si** Athumani.
c. Kalamu **i** mezani.

**VIELEZI (E)** (**Adverbs**)

Vielezi ni maneno yanayotoa habari zaidi kuhusu vitenzi, vivumishi au vielezi vingine.

**Aina za Vielezi**

**i. Vielezi vya Mahali**

Vielezi vya mahali hutoa habari kuhusu mahali ambapo kitendo kilifanyika. Aghalabu vielezi hivi huundwa kwa kutumia jina la mahali au kwa kuongeza kiungo -NI mwishoni mwa neno linaloashiria mahali. k.m: *nyumbani, kazini, shuleni*

Mtoto huyo hajatulia **nyumbani** tangu alipotoka **Mombasa**.

Msipitie **sokoni** mkienda **kanisani**.

**ii. Vielezi vya Wakati**

Huelezea zaidi kuhusu wakati kitendo kipofanyika. Kwa mfano: *jioni, jana, asubuhi, saa saba, mwaka juzi*

Mzee Kasorogani amesema kwamba ataoga **mwaka ujao.**

Musa alilazimishwa kuchimba mtaro **saa sita usiku.**

Kisaka na Musa watakutana **kesho**

**iii. Vielezi vya Idadi**

Vielezi vya idadi hutulezea kitendo kilifanyika mara ngapi.

***a) Idadi Kamili***

Vielezi vya Idadi Kamili hutaja idadi kamili ya mara ngapi kitendo kilifanyika. k.m: *mara mbili, siku mbili kwa juma, mara kumi*

Gibi alimzaba kofi **mara tatu** na kisha akakimbia.

Daktari alimwagiza mama huyo achukue dawa **mara tatu** kwa siku na arudi hospitalini siku **mbili kwa mwezi**

***b) Idadi Isiyodhihirika/isiyokamili***

Vielezi vya Idadi Isiyodhirika huelezea kiasi ambacho kitendo kilifanyika bila kutaja kiasi kamili k.m: *chache, nyingi, kadhaa, kidogo, wastani*

Mwizi wa kuku alipigwa **mara kadhaa** kabla ya kuokolewa na polisi.

Yeye hunipigia simu **mara kwa mara**

**iv. Vielezi Vya Namna**

Huelezea jinsi au namna kitendo kinavyofanyika. Kitendo kinaweza kufanyika kwa namna mbalimbali. Hivyo basi kuna aina mbalimbali za vielezi vya namna:

***a) Vielezi vya Namna Halisi***

Hutufahamisha jinsi kitendo kinavyofanyika kwa kutumia maneno halisi (bila kuambatanishwa na maneno mengine au viambishi vingine). k.m: *vizuri, ovyo, haraka*

Kioo cha bibi harusi kilianguka na kuharibika **vibaya.**

Mama alipika chakula **upesi.**

Amepigwa kalamu kwa kufanya kazi **kiholela**

***b) Vielezi vya Namna Hali***

Hutufahamisha hali ambayo kitendo kilifanyika. Vielezi hivi hujihusisha na tabia ya kitu/mtendaji wa kitendo. k.m: *kwa furaha, kwa makini,*

Bibi harusi aliingia kanisani **kwa madaha.**

Mtoto alilia **kwa maumivu** mengi

***c) Vielezi vya Namna Kitumizi/Ala***

Hutoa habari kuhusu kifaa, ala au mbinu iliyotumiwa kufanya kitendo fulani. k.m: *kwa kisu, kwa jembe, kwa meno, kwa moto, kwa maji*

Mkulima aliangusha mti mkubwa **kwa shoka.**
Mzee huyo alimpiga mke wake **kwa bakora** kabla ya kuchoma nguo zake **kwa makaa.**

**v. Vielezi Vikariri**

Husisitiza kitendo kinavyofanyika kwa kutaja kielezi kinachorejelewa mara mbili mfululizo. k.m: *haraka haraka, ovyo ovyo, juu juu*
Polisi walipoingia, wezi walitawanyika **haraka haraka**.
Wanafunzi wengi hufanya kazi yao **ovyo ovyo**

**vi. Vielezi vya Ki-Mfanano**

Vielezi mfanano hutumia KI-mfanano kuelezea kitendo kinavyofanyika kwa kulinganisha. k.m: *kitoto, kiungwana*
Babake huongea **kiungwana**.
Harida hutembea **kijeshi.**

**vii. Vielezi Viigizi**

Vielezi hivi huigiza sauti au mlio wa kitu, kitendo kilipofanyika kwa kutumia tanakali za sauti. k.m: *tuli, chubwi, tifu, chururu*
Mwanafunzi alitulia **tuli** mwalimu alipomzaba kofi **pa**!
Kaswimu aliangusha simu changaraweni **tifu** na kujitumbukiza majini **chubwi**

**viii. Vielezi vya Vielezi**

Vielezi hivi hutumika kuelezea kielezi kingine. Hivyo basi, hutanguliwa na kielezi badalaya kitendo k.m: *sana, kabisa, hasa, mno*
Mamake Kajino alitembea polepole **sana**.
Chungu kilivunjika vibaya **kabisa**

**ix. Vielezi vya Vivumishi**

Hutoa habari zaidi kuhusu kivumishi. Kwa mfano: *sana, kabisa, hasa, mno*
Yeye ni mrefu **sana.**
Mtoto wake ana tabia nzuri **mno**

## VIHUSISHI (H) (Prepositions)

Vihusishi ni maneno yanayotuarifu zaidi kuhusu uhusiano wa nomino na mazingira yake.

**Aina za Vihusishi**

**i. Vihusishi vya Mahali**

| **Kihusishi** | **Sentensi** |
|---|---|
| mbele ya/nyuma ya | Kuna mzoga **nyuma ya** jengo hilo. |
| chini ya/ juu ya | Joto lilipozidi watoto waliketi **chini ya** mti ule. |
| kando ya | **Kando ya** mito ya Babeli ndipo tulipoketi. |
| karibu na/mbali na | Fisi aliambiwa asile mifupa **karibu na** mtoto yule. |

**ii. Vihusishi vya Wakati**

| **Kihusishi** | **Sentensi** |
|---|---|
| kabla ya | Ni vizuri kusali **kabla ya** kula chakula. |
| Baada ya | Watoto safi hupiga meno mswaki **baada ya** kila mlo. |

**iii. Vihusishi vya kulinganisha**

Navyo ni; kama, kuliko

**TANBIHI:** Kiunganishi **'na'** kinapopatikana kati ya kitenzi na nomino au kati ya kitenzi na kiwakilishi hufanya kazi ya kihusishi. Kwa mfano:

d. Chakula kilipikwa **na** mama mkakamavu.
e. Gari linaendeshwa **na** yeye mwenyewe.
f. Ujenzi wa barabara nzuri utasimamiwa **na** taifa la uingereza.

## UYAKINISHI NA UKANUSHO

**Kukanusha** ni kukataa au kukana kauli. **Kuyakinisha** ni kuthibitisha/kukubali/kuhakikisha ukweli wa jambo.

Mara nyingi tunapokanusha, tuanaongeza kiambishi 'HA-' mwanzoni mwa kitenzi. Hata hivyo, kiambishi hicho hubadilika katika nafsi ya kwanza na ya pili umoja. Angalia jedwali lifuatalo.

| KIAMBISHI | MATUMIZI | MFANO |
|---|---|---|
| **SI** | nafsi ya kwanza | si-ku-wa-on-a |
| **HU** | nafsi ya pili | hu-ni-faham-u |
| **HA** | nafsi ya tatu | ha-ta-chuku-a |

**Kukanusha Wakati Uliopita (LI) => 'KU'**
1 Kajuta alimpigia kura. Kajuta hakumpigia kura.
2 Nilikupa nafasi yako. Sikukupa nafasi yako
**Kukanusha Wakati Timilifu (Uliopita Muda Mfupi) (ME) => 'JA'**
1 Maziwa ya nyanya yamemwagika. Maziwa ya nyanya hayajamwagika.
2 Viwete wametembea. Viwete hawajatembea.
**Kukanusha Wakati Uliopo (NA) => '-I'**
1 Unasoma sentensi ya kwanza. Husomi sentensi ya kwanza.
2 Zinafanana na nyota. Hazifanani na nyota.
**Kukanusha Wakati Ujao (TA) => 'TA'**
1 Jua litawaka sana. Jua halitawaka sana.
2 Watakaribishwa kwenye malango ya lulu. Hawatakaribishwa kwenye malango ya lulu.
**Kukanusha Wakati wa Mazoea (HU) => '-I'**
1 Polisi wa jiji kuu huchukua hongo. Polisi wa jiji kuu hawachukui hongo.
2 Bendera hufuata upepo. Bendera haifuati upepo.
**Kukanusha Wakati Usiodhihirika (A) => '-I'**
1 Anita ampenda Kaunda. Anita hampendi Kaunda.
2 Chema chajiuza, kibaya chajitembeza. Chema hakijiuzi, kibaya hakijitembezi.
**Kukanusha KI ya Masharti (KI) => 'SIPO'**
1 Ukimwadhibu mtoto, atapata adabu njema. Usipomwadhibu mtoto hatapata nidhamu.
2 Bei yake ikishuka, nitainunua. Bei yake isiposhuka, sitainunua.
**Kukanusha PO ya Wakati (PO) => 'SIPO'**
1 Uamkapo asubuhi ndugu yangu mshukuru Mungu. Usipo amka asubuhi ndugu yangu usimshukuru Mungu.
2 Mtoto aliapo mnyonyeshe. Mtoto asipo lia usimnyonyeshe
**Kukanusha Hali ya Uwezekano (NGE) => 'SINGE'**
1 Ningekuwa nakupenda ningekwambia mapema. Nisingekuwa nakupenda nisingekwambia mapema.
2 Zingekuwa nyingi, wangeziiba. Zisingekuwa nyingi, wasingeziiba.
**Kukanusha Hali ya Uwezekano (NGALI) => 'SINGALI'**
1 Khadija angalisoma kwa bidii angalikuwa na cheo kikubwa.- Khadija asingalisoma kwa bidii asingalikuwa na cheo kikubwa.
2 Yangalikuwa mabivu yangalianguka yenyewe. Yasingalikuwa mabivu yasingalianguka yenyewe

**Kukanusha Amri/Agizo (-a/-e) => 'SI'**
1 Peleka kikapu hiki kwa nyanya. Usipeleke kikapu hiki kwa nyanya.
2 Chakula kiliwe. Chakula kisiliwe.
3 Mpende adui yako. Usimpende adui yako.
4 Waambieni watu wa mataifa yote. Msiwaambie*ni* watu wa mataifa yote.
**Kukanusha Viunganishi vya Kujumuisha (NA, KA) => 'WALA'**
1 Bafi alikuzaba kofi na kukupiga teke. Bafi hakukuzaba kofi wala hakukupiga teke.
2 Mama amepika chakula tukala pamoja. Mama hajapika chakula wala hatujala pamoja

## VINYUME/ANTONIMU

**Kinyume cha Kawaida**
Kinyume ni neno ambalo hupingana kimaana na kimatumizi.
Kinyume hupatikana katika:

**Vitenzi**

**Vinyume amavyo hubadilisha kitenzi na kukiweka katika kauli ya kutendua.**

| Kitenzi | kinyume | kitenzi | kinyume |
|---|---|---|---|
| choma | chomoa | funga | fungua |
| ziba | zibua | waza | wazua |
| ganga | gangue | komea | komoa |
| chana | chanua | tia | toa |
| bana | banua | ezeka | ezua |
| pakia | pakua | fuma | fumua |
| panga | pangua | shona | shonoa |
| ficha | fichua | twika | tua |
| funika | funua | nasa | nasua |
| umba | umbua | tega | tegua |
| kunja | kunjua | vaa | vua |
| fukia | kukua | komea | komoa |
| kosa | kosoa | shona | shonoa |
| chimba | chimbua | | |

**vinyume ambavyo huwa maneno mengine tofauti na vitenzi asilia.**

| Kitenzi | Kinyume | Kitenzi | Kinyume |
|---|---|---|---|
| anza | maliza | ajiri | futa/achisha |
| bakiza | maliza | shikilia | achilia |
| uliza | jibu | paaza/zidisha | punguza |
| afikiana | hitilifiana/kosa | mwaga | zoa |
| kwea | shuka | oa | taliki |
| furahisha | huzunisha | ongoza | potosha |
| choshwa | pumzishwa | ugua | pona |
| chafua | safisha/takasa | zama | elea/ibuka |
| babaika | tulia | weza | shindwa |
| jenga | bomoa | kiri | kana |
| simama | keti/kaa | tii | asi/puuza |
| cheka | lia | onea | pendelea |
| lala | amka | tawanya | kusanya |
| pata | poteza | sema | nyamaza |
| panda | shuka | nuna | tabasamu |
| bariki | laani | lewa | leuka |
| nyesha | pusa/chesha | unga | kata |

**vivumishi**

| Kivumishi | Kinyume | Kivumishi | Kinyume |
|---|---|---|---|
| chema/kizuri | kibaya | chafu | safi |
| -fupi | -refu | -embamba | -nene |
| -ingi | -chache | -eusi | -eupe |
| mjuzi | limbukeni | -dogo | -kubwa |
| kaidi | tiifu | kavu | nyevu |

**Vihusishi**

**kinyme**

| | |
|---|---|
| mbele ya | nyuma ya |
| chini ya | juu ya |
| kabla ya | baada ya |
| mbali na | karibu na |

**Vielezi**

| | |
|---|---|
| haraka<br>kutwa | polepole/asteaste/tarabu<br>kuchwa |

## NYAKATI/NJEO NA HALI

### NYAKATI MBALIMBALI

Hutumika kuonyesha ni lini kitendo kilifanyika, kitafanyika au kinafanyika au hakitafanyika ukilinganisha na wakati wa uzungumzi, Njeo huonyesha wakati tukio au hali imetokea au haikutokea. Lugha ya Kiswahili ina aina tatu kuu za nyakati. *Wakati uliopita-**li**-*
*Wakati uliopo-**na**-*
*Wakati ujao-**ta**-*

**Wakati uliopita –li-**

Wakati huu hurejelea kitendo kilichofanyika muda mrefu uliopita na kutimia. Vitenzi katika wakati uliopita hutumia kiambishi **"li"**. Kwa mfano: *Ni**li**hudhuria warsha juma lililopita.*
*Mzee huyo a**li**fukuzwa kazini.*

**Wakati uliopo –na-**

Wakati uliopo huonyesha kitendo kinachoendele kufanyika sasa hivi. Hutumia kiambishi **"na"** katika vitenzi. Kwa mfano: *Maria a**na**cheza uwanjani.*
*Wanafunzi wa**na**kula bwaloni.*

**Wakati ujao –ta-**

Huchukua kiambishi **"ta"** na hurejelea kitendo ambacho bado hakijafanyika lakini kinatarajiwa kufanyika. Kwa mfano: *Omari a**ta**safiri kesho.*
*Kimeli a**ta**ondoka mtondogoo.*

**HALI MBALIMBALI**

Hali hueleza namna ya kutendeka kwa kitendo/njia tofauti tofauti za kutazama kutukia au kutendeka kwa tendo, jambo au hali fulani.

1. **Hali ya mazoea –hu-**

   Hutumia kiambishi **"hu-"** na hurejelea kitendo ambacho hufanyika mara kwa mara au kila siku hadi kikawa mazoea/desturi. Kwa mfano: *Juliana **hu**fika kazini mapema.* *Ng'ombe **hu**la nyasi.*

**Hali isiyodhihirika ya wakati uliopo –a-**

Hutumia kiambishi cha ngeli au nafsi pamoja na kiungo **"a"** kurejelea kitendo kinachoendelea kutendeka katika wakati uliopo hali isiodhihirika. Kwa mfano:*Wanafunzi **wa**msumbua mwalimu.*
*Daraja **la**sombwa na maji ya mvua.*

2. **Hali ya –ka-**

   Hutumia kiungo **"-ka-"** kurejelea kitendo ambacho kinakamilika katika wakati usiojulikana.

Hutumika kurejelea mfuatano wa vitendo au matukio.
*Mukami alitia embe kapuni li**ka**iva.*
Hutumiwa katika masimulizi pamoja na wakati uliopo kuonyesha mfululizo wa matukio.
*Mwalimu aliingia darasani, a**ka**wafundisha wanafunzi, a**ka**watahini, a**ka**sahihisha majibu yao kisha a**ka**arudi kwake.*
*Wanafunzi waliingia darasani, wa**ka**toa vitabu vya, wa**ka**fungua ukurasa fulani wa**ka**anza kusoma.*
Huonyesha kuwa kitendo fulani kinasababishwa na matokeo ya kingine.
*Wachezaji hao walifanya mazoezi mengi wa**ka**shinda mechi.*
*Wanakwaya hao waliimba vyema wa**ka**tuzwa.*
Kuonyesha matarajio ya kutendeka kwa kitendo fulani.
*Maria atapelekwa shuleni a**ka**pate masomo ya kumfaa.*
*Nitakwenda Mumias ni**ka**wahutubie walimu wa Kiswahili.*

Kuashiria ombi au rai.
***Ka**chezeni kule uwanjani!*

3. **Hali timilifu –me-**

Huonyesha kuwa tendo limetendeka na kukamilika lakini athari zake bado zinaonekana. Kwa mfano:
*Moto u**me**chema nyumba ya jirani.*
*Wanasiasa wa**me**maliza kampeni.*
Huweza kujitokeza katika nyakati zote tatu za Kiswahili kama vile:

**Wakati uliopo hali timilifu**

Kuonyesha kitendo kimekamilika wakati wa sasa/hakijakamilika wakati wa sasa. Kwa mfano:
*Kilunda a**me**kubali kuigiza jukwani.*
*Hali ya anga i**me**tulia.*

**Wakati uliopita hali timilifu**

Kitendo likamilika muda mrefu uliopita hata matokeo yake bado yanaonekana. Kwa mfano:
*Sarafina a**li**kuwa a**me**mwandalia mzazi.*
*Khasiani a**li**kuwa a**me**andaa shamba kwa ajili ya upanzi.*

**Wakati ujao hali timilifu**

Kitendo kinatarajiwa kufanyika na kukamilika wakati ujao/siku za usoni. Kwa mfano:
*Watahiniwa wa**ta**kuwa wa**me**maliza mitihani yao.*
*Upepo huo u**ta**kuwa u**me**tulia.*

4. **Hali ya kuendelea**

Kitendo kinatendeka au kimo katika hali ya kutendeka. Kuna nyakati zote vilevile:

**Wakati uliopo hali ya kuendelea**

Kitendo kinaendelea sasa. Kwa mfano:
*Wabunge wanajadili suala hilo.*
*Wanakamati wanaondoka mkutanoni.*

**Wakati ujao hali ya kuendelea**

Kitendo kinatarajiwa kuwa katika hali ya kutendeka wakati ujao. Kwa mfano:
*Mabasi ya**ta**kuwa ya**na**pakwa rangi/Mabasi ya**ta**kuwa ya**ki**pakwa rangi.*
*Wazazi wa**ta**kuwa wakilipa karo/wazazi hawa**ta**kuwa wa**na**lipa karo.*

**Wakati uliopita hali ya kuendelea**

Kitendo kilikuwa kikiendelea wakati uliopita. Kwa mfano:
*Mazingira ya**li**kuwa ya**na**nadhifishwa./Mazingira ya**li**kuwa ya**ki**nadhifishwa.*
*Barabara ilikuwa inaundwa./ barabara i**li**kuwa i**ki**undwa.*

5. **Hali ya masharti**

Hali ya vitendo viwili kutegemeana ambapo kufanikiwa kwa tukio moja husababisha kufanikiwa kwa tukio linguine/kutofanikiwa kwa tukio moja husababisha kutofanikiwa kwa linguine. Kwa mfano:
*Athmani a**ki**durusu vyema atapita Kiswahili.*
*Madaktari wa**sipo**ongezewa mishahara hawatarudi kazini.*

a) **–ki-**

Kuonyesha masharti ambayo yanawezekana ikiwa masharti fulani yatatimizwa. Kwa mfano:
*Lami i**ki**wekwa katika barabara hii wasafiri watafurahi.*
*Raia wakishirikiana na polisi usalama utaimarika.*

**b) –nge-, -ngeli- na –ngali-**

**-nge- na –ngeli-**

Masharti yanayowezekana: tukio halikutendeka wakati uliopita lakini bado kuna nafasi/matumaini/uwezekano wa sharti kutimizika/matukio kufanyika.

*Barasa a**nge**kuwa na pesa a**nge**kusaidia.*
*Kiti hicho ki**nge**kuwa mathubuti ki**nge**kaliwa.*

***Tanbihi:*** **-nge-** ikitumika katika usemi halisi huwakilisha **–ta-** ya wakati ujao.

**-ngali-**

Huashiria kuwa vitendo viwili vinavyotegemeana **havikutendeka wala hakuna matumaini/nafasi/uwezekano wa kufanyika.** Kwa mfano:

*Ngo'ombe a**ngali**lishwa vizuri angalitoa maziwa mengi.*
*Wakulima wa**ngali**panda mapema wa**ngali**vuna mazao.*

Hutumika kama kitenzi kisaidi au kitenzi kishirikishi kuonyesha **kitendo kinadumu**. Kwa mfano:

*Mhubiri **angali** kanisani.*

***Tanbihi:*** Ni makosa kuchanganya **–nge-, -ngeli-** na **–ngali-** katika kutunga sentensi moja. Kwa mfano:

**Makosa:** *Mwalimu a**nge**tufunza vyema tu**ngali**lielewa.*
**Sahihi:** *Mwalimu a**nge**tufunza vyema tu**nge**lielewa.*

**Au**

*Mwalimu a**ngali**tufunza vyema tu**ngali**lielewa.*

6. **Hali ya –po-**

Huashiria wakati maalum(ikiwa kiambishi cha kati). Kwa mfano:

*Wanyama wali**po**furushwa, walitoroka mwituni.*

Huonyesha wakati wowote(ikija mwishoni katika kitenzi). Kwa mfano:

*Mwalimu afika**po** darasani, msikilize kwa makini.*

7. **Hali ya kuamuru**

Huashiria kuamrisha au kushurutisha mtu au kitu kinachotendewa jambo.

Katika umoja/ukiamrisha mtu mmoja, usiongeze viambishi vya nafsi katika vitenzi. Kwa mfano*Lala! Oga!*

Kwa vitenzi vya silabi moja, ambisha **ku-** awali. Kwa mfano:***Ku**la! **Ku**nywa!*Katika wingi ambisha **–ni** baada ya vitenzi vya asili ya kigeni lakini ambish **–ni** baada ya kiambishi **–e-** cha nia ya kutenda kwa vitenzi vya asili ya Kibantu. Kwa mfano:

**Kibantu**

*Kimbi- kimbi**eni***
*Lala- lal**eni***
*Cheza- chez**eni***

**Kigeni**

*Samehe- samehe**ni***
*Tubu- tubu**ni***

8. **Hali ya uezekano wa jambo**

Pale ambapo kitendo hakijafanyika ila kinatarajiwa kufanyika. Kwa mfano:

***Huenda** wageni wakawasili leo*

**MNYAMBULIKO WA VITENZI VYA SILABI MOJA**

Hivi ni vitenzi ambavyo shina lake lina silabi moja pekee. Ili kuleta maana kamili, vitenzi hivi huambatanishwa na kiungo **"ku-"** mwanzoni ili viweze kueleweka. Kwa mfano; **kula.** Kiambishi hicho hudondoshwa vitenzi vinaponyambuliwa katika hali nyingine.

Kama vitenzi vingine, vitenzi vya silabi moja vinaweza kunyambuliwa.mifano ya vitenzi hivi ni:

**1. Cha(kucha)**-jua kuchomoza/kuwa asubuhi/pambazuka: ***kumekucha***

-kuogopa/kumwogopa Mungu- ***kumcha Mungu si kilemba cheupe.***

**Mnyambuliko:**

| **Kutenda** | **kutendea** | **kutendesha** | **kutendama** | **kutendeana** |
|---|---|---|---|---|
| **Cha** | chia/chelae | chisha | chana | chiana |

*Walevi **walichewa** na jua barabarani walikolala usiku **kucha.***
*Miujiza **huwachisha** watu wengi sana.*
***Mchelea** mwana kulia hulia yeye.*
*Tunapoamka hupenda kuangalia kule jua **huchelea.***
*Majogoo hayo **yanachiana** tangu yapigane.*

**2) fa(kufa)** -kuacha kupumua, kupoteza/kukosa/tokuwa hai.

**Mnyambuliko:**

| **Kutenda** | **kutendea** | **kutendwa** | **kutendesha** | **kutendeana** |
|---|---|---|---|---|
| **Fa** | fia | fiwa | fisha | fiana |

*Baba yetu **alipokufa** tulilia sana.*
***Tulipofiwa** na baba yetu, tulilia sana.*
*Wakristo wanaamini kuwa, Yesu **aliwafia** msalabani ili wasamehewe dhambi. (**kwa niaba yao**)*
*Watu wengi **wamefia** Salgaa wakiwa safarini.(**mahali pa kifo kutokea**)*
*Ugonjwa wa saratani **huwafisha** watu wengi kisirisiri. (**husababisha watu kufa**)*

**3) ja(kuja)** -fika mahali hapa/wasili.
-Pia huleta dhana ya kuingia katika hali fulani.

**Mnyambuliko:**

| **Kutenda** | **kutendea** | **kutendewa** | **kutendeana** |
|---|---|---|---|
| **Ja** | jia | jiwa | jiana |

*Naibu wa mwenyekiti **alimjia** mwenyekiti mkutanoni wakati mwenyekiti alikuwa safarini.(**niaba ya**)*
*Morasi **alikuja** jana kutoka Kisii.*
*Ukitukana watu wazima **utakuja** kupigwa.*
*Jana jioni **nilijiwa** na wageni kutoka nyumbani kwetu.*
*Mimi na rafiki yangu **tulijiana** karamuni.*

**4) La(kula)** -kutia chakula mdomoni na kumeza.
-Pia ina maana ya kutumia kitu.

**Mnyambuliko:**

| **Kutenda** | **kutendea** | **kutendewa** | **kutendesha** | **kutendeana** | **kutendeka** |
|---|---|---|---|---|---|
| **La** | lia | liwa | lisha | liana | lika |

*Mbwa hupenda **kula** kinyesi.*
*Laban **amekula** pesa zote kwa anasa.(**kutumia kitu**)*

**5) Nya(kunya)** -Kutoa mabaki ya chakula toka tumboni/enda haja kubwa.
-Toa kitu majimaji.

**Mnyambuliko:**

| **Kutenda** | **kutendea** | **kutendewa** | **kutendesha** | **kutendeana** | **kutendeka** |
|---|---|---|---|---|---|
| **Nya** | nyia/nyea | nyiwa/nyewa | nyesha | nyiana | nyika |

*Mvua **hunya** katika maeneo ya Ziwa Viktoria.*
*Mvua **inawanyea** wanafunzi wakitoka shuleni.*
*Mtoto **amenyea** sahani ya chakula.*
*Mawingu hutanda maeneo ya Garissa kisha mvua **hunyesha** maeneo ya Mombasa.*
*Kufukuzwa na samba **kulimnyesha** Fardosa.(**kulimfanya Fardosa kuenda haja kubwa**) Mtoto **alinyewa** na ndege alipokuwa amelazwa chini ya mti.*

**6) Nywa(kunywa)** -ingiza mdomoni na kumeza kitu majimaji/pata kinywaji/sharabu.

**Mnyambuliko:**

| Kutenda | kutendea | kutendewa | kutendesha | kutendeshana | kutendeka |
|---|---|---|---|---|---|
| **Nywa** | nywea | nywewa | nywesha | nyweshana | nyweka |

*Walimu **wamekunywa** chai.*
*Mulinge **ataninywea** maziwa yangu; siyataki.(**kwa niaba ya**)*
***Tutanywea** chai Nakuru wakati tutakaposafiri kwenda Gilgil.(**mahali**)*
*Sharubati **hunyweka** hata wakati wa barudi.*
*Maji yangu ya kuoga **yalinywewa** na kondoo wa jirani.*
*Bibi arusi **alimnywesha** bwana arusi divai.*
*Wapenzi wale **wananyweshana** soda hadharani.*

**7) Pa(kupa) -**kabidhi kitu kwa mtu mwingine/toa mtu au kitu kwa mtu mwingine ili apokee au apate.
**Mnyambuliko:**

| Kutenda | kutendea | kutendewa | kutendesha | kutendeana | kutendeka |
|---|---|---|---|---|---|
| **Pa** | pea | pewa | pasha | peana | peka |

*Mtalii **alinipa** zawadi baada ya kumwonyesha njia.*
*Mama **alinipea** mtoto wangu maziwa nilipokuwa nimesafiri.(**kwa niaba yangu**) Wachezaji **walipewa** sare ya michezo.*
*Walimu na wazazi **walipeana** zawadi katika hafla hiyo.(**kila kikundi kilitoa zawadi kwa kingine**)*
*Rushwa ndio **hupeka** kila mahali nchini mwetu.(**inatolewa kwa urahisi na kupokelewa**) Mkurugenzi **ametupasha** habari nzuri kuhusu mishahara.(**amefanya tupate ujumbe kwa kutuarifu**)*

**8) Pwa(kupwa) -**Hali ya maji kutoka ufukoni na kwenda/kuhama na kwenda mpaka sehemu ya mbali ya bahari; kinyume na kujaa.
**Mnyambuliko:**

| Kutenda | kutendea | kutendewa | kutendeka |
|---|---|---|---|
| **Pwa** | pwea | pwelewa | pweka |

*Bahari **imekupwa** sasa, twende tutembee ufukoni.*
*Samaki **wamepwelewa** baada ya maji ya ziwa kupunguka.(**kwama nchi kavu**)*

**9) Chwa(kuchwa) -**jua linapozama/kutua kwa jua magharibi/usiku kuingia.
**Mnyambuliko:**

| Kutenda | kutendea | kutendewa | kutendeka |
|---|---|---|---|
| **Chwa** | chwea/chwia | chwewa | chweka |

*Tumekaa hap asana hadi **kumekuchwa;** heri tuondoke sasa.*
*Jua **limetuchwea** barabarani kabla tufike Mombasa; itabidi tulale hapa hadi asubuhi.*
***Tulichwewa/tulichwiwa** na jua mjini Naivasha tukaamua kukatiza safari mpaka siku ambayo ingefuata.*

**10) Wa(kuwa) -**kutokea katika hali au mahali fulani/baki katika hali ileile au palepale.
**Mnyambuliko:**

| Kutenda | kutendea | kutendewa | kutendeana |
|---|---|---|---|
| **Wa** | wia | wiwa | wiana |

*Sara **alikuwa** Urusi hadi uzeeni mwake.*
*Salim **amekuwa** pwaguzi mkubwa sana siku hizi.*
*Maisha **yalimwia** magumu kutokana na unywaji wake wa pombe.*
*Mwizi alimwomba jaji **kumwia** radhi kwa kosa la wizi na kuahidi kutorudia.*
*Msichana aliyemtusi mwenzake **amewiwa** radhi na chifu wa kata yake.*
*Waislamu wanapasa **kuwiana** radhi kila wanapokosana*

## SENTENSI YA KISWAHILI

### MUUNDO WA SENTENSI

**Sentensi** ni utungo unaoeleza dhana iliyokamilika kwa kushirikisha **kiima** na **kiarifu/kiarifa**.

Lugha ya Kiswahili ina sentensi za aina mbalimbali: zenye muundo rahisi, mwepesi na zenye muundo usiokuwa rahisi.

**Kiima** huwa nomino ya mtendaji wa kitendo. Yaani, nomino inayofanya tendo.
**Kiarifa/kiarifu** huwa kitenzi kinachotendwa na kiima.

**Sifa za sentensi**
a) Huwa na ujumbe uliokamilika.
b) Huwa na mpangilio maalum wamaneno.
c) Huwa na muundo wa kiima na kiarifu.

**Aina za sentensi**
**Sentensi Sahili**
Sentensi ambayo huwa na kitenzi kimoja(wazo moja kuu). Ni sentensi rahisi au nyepesi.
**Sifa**
a) Huwa fupi.
b) Huwa na kitenzi kimoja pekee.
c) Huwasilisha dhana moja.
d) Yaweza kuwa ya neno moja au zaidi.
**Mifano:**
*Wataenda.*
*Watotowawiliwanaelekeauwanjani.*
*Gachikunimsichanamtiifu.*
**Sentensi Ambatano**
Inayoundwa kwa kuunganisha sentensi sahili mbili.
**Sifa**
a) Huwa na vishazi huru viwili.
b) Huwa na kiunganishi.
c) Huwa na vitenzi viwili au zaidi.
d) Hutoa zaidi ya wazo moja.
e) Yaweza kuwa na viima vilivyododoshwa.
**Mifano:**
*Mwanafunzi alipita mtihani ingawa hakuwa anasoma kwa bidii.*
*Maria aliendelea kupika kwa utaratibu huku akiimba wimbo.*
**Sentensi Changamano**
Ni sentensi ambayo huwa na kishazi tegemezi kilichochopekwa ndani.
**Sifa**
a) Huwa na kishazi tegemezi chenye kitenzi kinachovumisha nomino kwa kuirejelea.
b) Huwa na kishazi huru kimoja au zaidi.
c) Huwa na virejeshi(ambana O) au –enye.
**Mifano:**
*Tunda alilonunua jana limeoza.*
*Mwizi aliiba pesa zilizokuwa kabatini.*

## NGELI ZA KISWAHILI

**Ngeli** ni **vikundi** vya majina ya Kiswahili. Katika mfumo wa kisasa (na unaokubalika), ngeli huundwa kwa kuunganisha viambishi viwakilishi vya nomino.
**Kwa mfano**, neno *kitabu*. Tunasema, *"Kitabu **ki**mepotea - Vitabu **vi**mepotea."* Kwa kuunganisha kiambishi "KI"(umoja) na VI(wingi), tunapata ngeli ya KI-VI.
Ni muhimu kusisitiza kwamba tunazingatia viambishi, wala si silabi ya kwanza. Hivyo basi, maneno yasioyoanza kwa KI-VI kama vile *chama -vyama* yatakuwa katika ngeli ya KI-VI kwa kuwa yanachukua kiambishi KI => (*Chama **ki**mevunjwa - Vyama **vi**mevunjwa.*)
Vivyo hivyo, kunayo majina yanayoanza kwa KI-VI yasiyokuwa katika ngeli ya KI-VI maadam yanachukua viambishi tofauti. k.v: kijana => A-WA (*kijana **a**mefika- vijana **wa**mefika*).

Tumekuandalia majedwali matatu kukupa mukhtasari wa ngeli zote za Kiswahili na jinsi baadhi ya maneno/viambishi vinavyobadilika kutoka ngeli moja hadi nyingine.

a) **Jedwali la kwanza linakupatia ngeli, maelezo yake, na mifano ya majina:**

| Ngeli | Maelezo | Mifano |
|---|---|---|
| A-WA | Hii ni ngeli ya majina ya viumbe wenye uhai k.v watu, wanyama, ndege, wadudu, miungu, malaika n.k<br>Majina **mengi** katika ngeli ya A-WA huanza kwa sauti M- kwa umoja na sauti WA- kwa wingi.<br>Hata hivyo baadhi ya majina huchukua miundo tofauti. | mtu-watu |
| KI-VI | Hii ni ngeli ya majina ya viumbe wenye uhai k.v watu, wanyama, ndege, wadudu, miungu, malaika n.k Majina mengi katika ngeli ya A-WA huanza kwa sauti M- kwa umoja na sauti WA- kwa wingi. Hata hivyo baadhi ya majina huchukua miundo tofauti. | kitu-vitu |
| LI-YA | Hujumuisha majina ya vitu visivyo hai pamoja na yale ya ukubwa k.v jitu.<br>Majina yake huchukua miundo mbalimbali. Baadhi yake huchukua muundo wa JI-MA (jicho-macho), lakini yanaweza kuanza kwa herufi yoyote.<br>Kwa wingi, majina haya huanza kwa MA- auME-. | jina-majina |
| U-I | Huwakilisha majina ya vitu visivyo hai, yaanzayo kwa sauti M- (umoja) na MI(wingi). | mti-miti |
| U-ZI | Hurejelea majina ambayo huanza kwa U- (umoja) na huchukua ZI- (wingi) kama kiambishi kiwakilishi cha ngeli katika wingi.<br>Majina yenye silabi tatu au zaidi hubadilishwa kwa wingi kwa kutoa sauti /u/' k.v ukuta - kuta.<br>Majina ya silabi mbili huongezewa /ny/ katika wingi. k.v ufa – nyufa. | ukuta-kuta |
| I-ZI | Hutumiwa kwa majina yasiyobadilika kwa umoja wala kwa wingi lakini huchukua viambishi viwakilishi tofauti:<br>I- (umoja) na ZI- (Wingi). Mengi yake huanza kwa sauti /u/, /ng/, /ny/, /mb/, n.k | nyumba-nyumba |
| U-YA | Ni majina machache mno yanayochukua kiambishi U(umoja) na YA(wingi). | uyoga-mayoga |
| YA-YA | Hii ni ngeli ya vitu visivyoweza kuhesabika (nomino za wingi). Hayana umoja. Mengi ya majina haya huanza kwa MA- lakini yanaweza kuchukua muundo wowote. | maji |
| I-I | Ni ngeli ya majina ya wingi ambayo huchukua kiambishi I- kwa umoja na pia kwa wingi. Majina haya hayana muundo maalum. | sukari |
| U-U | Majina ya nomino za wingi yanayoanza kwa sauti /u/ au /m/. Hayana wingi. | unga |
| PA-PA | Ni ngeli ya mahali/pahali - maalum. | mahali |
| KU-KU | Ngeli ya mahali - kwa ujumla. Aidha, hujumuisha nomino za kitenzi-jina | uwanja |
| MU-MU | Ngeli ya mahali - ndani. | shimo |

b) **Jedwali la pili linaangazia jinsi ngeli mbalimbali zinavyotumia "a-nganifu", viashiria na viashiria visisitizi.**

| NGELI | A-UNGANIFU | VIASHIRIA | | | VIASHIRIA VISISITIZI | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | **KARIBU** | **MBALI KIDOGO** | **MBALI** | **KARIBU** | **MBALI KIDOGO** | **MBALI** |
| A-WA | wa-wa | huyu-hawa | huyo-hao | Yule-wale | uyu-huyu wawa-hawa | uyo-huyo ao-hao | Yule-yule wale-wale |
| KI-VI | cha-vya | hiki-hivi | hicho-hivyo | kile-vile | kiki-hiki vivi-hivi | chicho-hicho vivyo-hivyo | kile-kile vile-vile |
| LI-YA | la-ya | hili-haya | hilo-hayo | lile-yale | ili-hili yaya(aya)-haya | ilo-hilo yayo(ayo)-hayo | lile-lile yale-yale |
| U-I | wa-za | huu-hii | huo-hiyo | ule- ile | uu-huu ii-hii | uo-huo iyo-hiyo | ule-ule ile-ile |
| U-ZI | ya-za | huu-hizi | huo-hizo | ule-zile | uu-huu izi-hizi | uo-huo izo-hizo | ule-ule zile-zile |
| I-ZI | wa-za | hii-hizi | hiyo-hizo | ile-zile | ii-hii izi-hizi | iyo-hiyo izo-hizo | ile-ile zile-zile |
| U-YA | wa ya | huu-haya | huo-hayo | ule-yale | uu-huu yaya(aya)-haya | uo-huo yayo(ayo)-hayo | ule-ule yale-yale |
| YA-YA | ya | haya | hayo | yale | yaya-haya | yayo-hayo | yale-yale |
| I-I | ya | hii | hio | ile | ii-hii | io-hio | ile-ile |
| U-U | wa | huu | huo | ule | uu-huu | uo-huo | ule-ule |
| PA-PA | pa | hapa | hapo | pale | papa-hapa | papo-hapo | pale-pale |
| KU-KU | kwa | huku | huko | kule | kuku-huku | kuko-huko | kule-kule |
| MU-MU | mwa | humu | humo | mle | mumu-humu | mumo-humo | mle-mle |

c) **Jedwali la tatu linaangazia virejeshi(-o, amba-, -enye, -enyewe), ote, o-ote, ingi, ingine n.k kulingana na ngeli mbalimbali.**

| NGELI | 'O' REJRSHI | AMBA | ENYE | ENYEWE | OTE | O-OTE | INGI | INGINE |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| A-WA | ye-o | ambaye-ambao | mwenye-wenye | mwenyewe-wenyewe | wote | yeyote-wowote | wengi | mwingine-wengine |
| KI-VI | cho-vyo | ambacho-ambavyo | chenye-vyenye | chenyewe-vyenyewe | chote-vyote | chochote-vyovyote | kingi-vingi | kingine-vingine |
| LI-YA | lo-yo | ambalo-ambayo | lenye- yenye | lenyewe-yenyewe | lote- yote | lolote-yoyote | jingi mengi | jingine-mengine |

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| U-I | o-yo | ambao-ambayo | wenye-yenye | mwenyewe-yenyewe | wote- yote | wowote-yoyote | mwingi-mingi | mwingine-mingine |
| U-ZI | o-zo | ambao-ambazo | wenye-zenye | wenyewe-zenyewe | wote- zote | wowote-zozote | mwingi-nyingi | mwingine-nyingine |
| I-ZI | yo-zo | ambayo-ambazo | yenye-zenye | yenyewe-zenyewe | yote- zote | yoyote-zozote | nyingi-nyingi | nyingine-nyingine |
| U-YA | o-yo | ambao-ambayo | wenye-yenye | wenyewe-yenyewe | wote- yote | wowote-yoyote | mwingi-mengi | mwingine-mengine |
| YA-YA | yo | ambayo | yenye | yenyewe | yote | yoyote | mengi | mengine |
| I-I | yo | ambayo | yenye | yenyewe | yote | yoyote | nyingi | nyingine |
| U-U | o | ambao | wenye | mwenyewe | wote | wowote | mwingi | mwingine |
| PA-PA | po | ambapo | penye | penywe | pote | popote | | pengine |
| KU-KU | ko | ambako | kwenye | kwenyewe | kote | kokote | kwingi | kwingine |
| MU-MU | mo | ambamo | mwenye | mwenyewe | mote | momote | | mwingine |

## UMOJA NA WINGI

Sentensi za Kiswahili zinaweza kubadilishwa kutoka kwa umoja hadi wingi, kulingana na ngeli yake. Baadhi ya ngeli hubaki sawia katika umoja na wingi.

**Mifano ifuatayo itakuonyesha umoja na wingi wa sentensi katika ngeli mbalimbali.**

**NGELI YA A-WA**

**Umoja:** Mlokole huyo ni mtiifu sana.
**Wingi:** Walokole hao ni watiifu sana.
**Umoja:** Mwanafuzi aliyefuzu vyema amepata ufadhili.
**Wingi:** Wanafunzi waliofuzu vyema wamepata ufadhili.

**NGELI YA KI-VI**

**Umoja:** Kioo chake kinang'ara.
**Wingi:** Vioo vyenu vinang'ara.
**Umoja:** Chakula kile kina mafuta mengi.
**Wingi:** Vyakula vile vina mafuta mengi.

**NGELI YA LI-YA**

**Umoja:** Jicho lake linamuuma.
**Wingi:** Macho yake yanamuuma.
**Umoja:** Tawi la mti huo limeanguka.
**Wingi:** Mata ya miti hiyo yameanguka.

**NGELI YA U-I**

**Umoja:** Mti huo huzaa matunda mengi.
**Wingi:** Miti hiyo huzaa matunda mengi.
**Umoja:** Mkebe uliotoboka una manufaa tele.
**Wingi:** Mikebe iliotoboka ina manufaa tele.

**NGELI YA U-ZI**

**Umoja:** Uzi wake umekatika.
**Wingi:** Nyuzi zao zimekatika.
**Umoja:** Ukutu uliobomoka umekarabatiwa na fundi.
**Wingi:** Kuta zilizobomoka zimekarabatiwa na fundi.

**NGELI YA I-ZI**

**Umoja:** Barabara iliyosakafiwa haisababishi ajali.
**Wingi:** Barabara zilizosakafiwa hazisababishi ajali.
**Umoja:** Pikipiki iliyonunuliwa imeharibika.
**Wingi:** Pikipiki zilizonunuliwa zimeharibika.

**NGELI YA U-YA**

**Umoja:** Ugonjwa uliyomsumbua sana umepata tiba.
**Wingi:** Magonjwa yaliyomsumbua sana yamepata tiba.
**Umoja:** Uwele uliopandwa mwaka jana umevunwa.
**Wingi:** Mawele yaliyopandwa mwaka jana yamevunwa.

**NGELI YA YA-YA**

**Umoja:** Maziwa yaliyochemshwa huwa na virutubishi muhimu.
**Wingi:** Maziwa yaliyochemshwa huwa na virutubishi muhimu.
**Umoja:** Maudhui yaliyojadiliwa na mwalimu yalitunufaisha.
**Wingi:** Maudhui yaliyojadiliwa na mwalimu yalitunufaisha.

**NGELI YA I-I**

**Umoja/Wingi:** Chunvi iliyonunuliwa jana imeisha.
**Umoja/Wingi:** Hewa tunayopumua ni ya bure.

**NGELI YA U-U**

**Umoja:** Uhasama uliokuwa umeshamiri kijijini umepungua.
**Wingi:** Uhasama uliokuwa umeshamiri kijijini umepungua.

**NGELI YA MAHALI(PA-KU-MU)**

**PA:** **Umoja:** Mahali ambapo pana maua panapendeza sana.
**Wingi:** Mahali ambapo pana maua panapendeza sana.
**KU:** **Umoja:** Mahali ambako kulipandwa maua kunapendeza sana.
**Wingi:** Mahali ambako kulipandwa maua kunapendeza sana.
**MU:** **Umoja:** Mahali ambamo mlipandwa maua mnapendeza sana.
**Wingi:** Mahali ambamo mlipandwa maua mnapendeza sana.

**MASWALI YA KCSE**

**2006**:
Andika kwa wingi (alama 1)
Nyundo hii imevunjika mpini wake.

**2008**:
Andika kwa wingi. (alama1)

Mvua imebomoa nyumba ya jirani.

**2014**:
Andika sentensi ifuatayo katikaumoja. (alama 2)
Hao wenyewe hawakuzingatia mafunzo ya lishe bora.

**2015**:
Andika sentensi ifuatayo katika umoja. (alama 1)
Mkihifadhi nafaka hizo vizuri maeneo haya yatakuwa na vyakula vya kutosha.

**2017**:
Andika sentensi ifuatayo katika umoja. (alama 1)
Maseremala walizilainisha mbao hizo wakatengenezea meza.

**2018**:
Andika sentensi ifuatayo katika wingi. (alama 1)
Nahodha alilihepa jabali hio, chombo kikafika ufuoni salama.

**2019**:
Andika sentensi ifuatayo katika wingi. (alama 1)
Seremala aliulainisha ubao huo ili kutengeneza kasha amuuzie mlinzi huyo.

**2020**:
Andika sentensi ifuatayo katika umoja. (alama 1)
Nyua walizojenga hapa zimesaidia kukabiliana na wahalifu hao.

## UKUBWA NA UDOGO

Nomino za Kiswahili huwa na maumbo mbalimbali:
-Kawaida/wastani
-Ukubwa
-Udogo

| **Wastani** | **Ukubwa** | **Udogo** |
|---|---|---|
| Kisu | jisu | kijisu |
| Mbuzi | buzi | kibuzi |
| Chupa | jichupa | kichupa |

**Ukubwa**

Nomino katika hali ya ukubwa huwekwa katika ngeli ya LI/YA. Maneno yenye mzizi wa silabi moja hungezwa **"ji"** au **"j"** mwanzoni katika mzizi huo kuyaweka katika ukubwa.

**M**tu **ji**tu
**Ki**ti **ji**ti
**M**ti **ji**ti
**Ki**su **ji**su
**M**to **ji**to

Maneno yenye mzizi wa silabi zaidi ya moja huchukua mzizi huo huo kuwa ukubwa wa hiyo nomino.

M-fupa fupa
n-gamia gamia
n-dege dege
m-lango lango
m-toto toto
n-guo guo
ki-kombe kombe
m-kono kono
m-buzi buzi
m-guu guu
ki-dole dole
n-gozi gozi

Nomino ambazo hazibadili maumbo katika umoja na wingi huwekwa katika ukubwa kwa kuongeza kiambishi awali **"ji-".**

Sahani jisahani
Meza jimeza
Barua jibarua
Baiskeli jibaiskeli

Nomino zenye sauti mwambatano katika mianzo yao hudondosha sauti hizo na kuchukua kiambishi **'j-'**Mwana jana

Mwizi jizi
Chungu jungu
Nyoka joka
Njia jia
Mwari jari
Mke jike
Nyundo jundo
Nyumba jumba
Mwanafunzi janafunzi

Nomino ambazo tayari zi katika ngeli ya LI-YA au huanza kwa kimbishi **"ji-"** huongezwa kiambishi awali **"ji-"**

Jicho jijicho
Jiwe jijiwe

| | |
|---|---|
| Tawi | jitawi |
| Duka | jiduka |
| Jino | jijino |
| Gari | jigari |
| Shamba | jishamba |
| Blanketi | jiblanketi |

**UDOGO**

Nomino zikiwekwa katika udogo huingia katika ngeli ya KI-VI.
Nomino katika ukubwa huongezwa kiambishi awali **"ki-"** kuziweka katika hali ya udogo umoja na kiambishi **"vi-"** kuzieka katika hali ya udogo wingi.

| Wastani | ukubwa | udogo umoja | udogo wingi |
|---|---|---|---|
| Mtu | jitu | kijitu | vijitu |
| Kiti | jiti | kijiti | vijiti |
| Mti | jiti | kijiti | vijiti |
| Kisu | jisu | kijisu | vijisu |
| Mto | jito | kijto | vijito |
| Mfupa | fupa | kifupa | vifupa |
| Ndege | dege | kidege | videge |
| Mlango | lango | kilango | vilango |
| Mtoto | toto | kitoto | vitoto |
| Nguo | guo | kiguo | viguo |
| Mkono | kono | kikono | vikono |
| Mguu | guu | kiguu | viguu |
| Sahani | jisahani | kijisahani | vijisahani |
| Meza | jimeza | kijimeza | vijimeza |
| Barua | jibarua | kijibarua | vijibarua |
| Baiskeli | jibaiskeli | kijibaiskeli | vijibaiskeli |
| Duka | jiduka | kijiduka | vijiduka |
| Mwizi | jizi | kijizi | vijizi |
| Chungu | jungu | kijungu | vijungu |
| Nyoka | joka | kijoka | vijoka |
| Njia | jia | kijia | vijia |

**Tanbihi:**
**i)** Kuna baadhi ya nomino haziwezi kugeuzwa katika hali ya ukubwa wala udogo. **Kwa mfano**; Nomino ambazo ziko katika ngeli ya I/I, KU na YA/YA.
**ii)** Si lazima nomino zingine ziwekwe katika udogo au ukubwa. Ukizilazimisha huenda ukazua majina ya ajabu.

**TANBIHI:** Njia hizo zilizotajwa hapo juu ni baadhi tu ya njia za kuweka nomino katika hali ya ukubwa na udogo, **Ila,** kuna njia nyingine ambazo hutumika kuweka maneno katika ukubwa na udogo.

## USEMI HALISI NA USEMI WA TAARIFA

**USEMI HALISI**

Ni kuandika kauli kwa kunukuu maneno halisi ambayo mtu alitamka mwenyewe/kama yalivyosemwa na mtu mwingine. Kwa mfano:

- **i)** malulu alisema, "Wanafunzi wote lazima wapate elimu."
- **ii)** "Kitabu hicho ni kikubwa, hutamaliza kukisoma." Mwalimu akasema.

**Zingatia haya unapoandika katika usemi halisi:**

1. **Alama za mtajo/nukuu hutumika kufungia maneno halisi ya msemaji.** Kwa mfano;

Kilelu alisema, “muhula huu ni mrefu sana.”

2. **Unaweza kutumia alama za nukta pacha badala ya alama za mtajo baada ya jina la msemaji.** Kwa mfano;
   **Ali:** Siku hizi mashambulizi yanayotekelezwa na magaidi yamezidi.
   **Hamedi:** Hali ya usalama imezorota hadi watu wanaogopa hata kuogopa.
3. **Kila neno la mwanzo la usemi halisi sharti lianze kwa herufi kubwa hata ikiwa usemi huo unakuja katikati mwa sentensi kuu.** Kwa mfano;
   Mwalimu alisema, “Bidii huleta mafanikio.”
4. **Alama za mtajo huwa mbili mbili(“ ”). Hata hivyo unaweza kutumia alama moja moja(‘ ’) ikiwa una nukuu ndogo ndani ya nukuu kubwa.** Kwa mfano;
   i. Mpishi alisema, “Leo itabidi mle ‘githeri’ kwa vile hatukupa mboga za kuundia sima.”
   ii. Daktari alimwambia, “Nilikuambia umeze dawa kama ulivyoagizwa! Ulisahu walivyosema wahenga kuwa ‘asiyesikia la mkuu huvunjika guu’?”
5. **Ikiwa msemaji atakatiza kauli kwa maneno mengine kisha aendelee, alama za mtajo zianatumika katika maneno hayo anayendelea kusema ila neno la kwanza la maneno hayo halitaanza kwa herufi kubwa.** Kwa mfano;
   “Bidii ni muhimu maishani,” akasema Mwanja, “ukijibidiisha utafaulu.”
6. **Alama za viulizi au hisi huwekwa ili kudhihirisha hisia.** Kwa mfano;
   “Unataka usaidiwaje?” Kakangu alisaili.
   “Ehe! Ulifikiri utafaulu?” Mwalimu alimwambia.
7. **Wakati uliopo hutumika.** Mfano;
   “Naona ni vyema muondoke mapema sasa,” kasisi aliwashauri.
8. **Viambishi vya nafsi ya msemaji hutumika.** Kwa mfano;
   “Nitahudhuria semina ya Mombasa,” Mwalimu alisema.

**<u>USEMI WA TAARIFA</u>**

Usemi unaorejelea kauli iliyotolewa na mtu mwingine bila kutumia maneno yale yale ya msemaji.

**Zingatia haya unapoandika katika usemi halisi:**

1. **Maneno halisi ya mtu hayatumiwi.** Kwa mfano;
   **Usemi halisi:** **“**je, mmeleta yale matofali niliyotaka?**”** Kilonzo aliwauliza.
   **Usemi wa taarifa:** Kilonzo alitaka kujua(aliwauliza) kama walikuwa wameleta(walileta) yale matofali aliyotaka.
2. **Ujumbe halisi wa msemaji unafaa kudumishwa katika usemi huu hata kama maneno halisi hayatumiwi.**
   **Usemi halisi:** Bakari alisema, “Nitawahudumia watu wote ipasavyo.”
   **Usemi wa taarifa:** Bakari alisema kuwa (kwamba) angewahudumia watu wote ipasavyo.
   **AU**
   Bakari aliahidi kuwahudumia watu wote ipasavyo.
3. **Alama za nukuu huondolewa.**
   **Usemi halisi:** **“**Wafundishe wanafunzi kwa roho moja ili ubarikiwe na Mungu,” shekhe aliwaambia walimu.
   **Usemi wa taarifa:** Shekhe aliwaambia walimu wafundishe wanafunzi kwa roho moja ili wabarikiwe na Mungu.
4. **Alama za kuuliza na za hisihuondolewa.**
   **Usemi halisi:** “Mnaenda wapi usiku huu?” Askari akawauliza.
   **Usemi wa taarifa:** Askari alitaka kujua walikokuwa wakienda usiku huo.
   **AU**
   Askari alwauliza walikokuwa wakienda usiku huo.
   **Usemi halisi:** “Lo! Moto umemchoma!” Mama alisema.
   **Usemi wa taarifa:** Mama alishangaa kuwa moto ulikuwa umemchoma.
   **AU**
   Mama alimaka kuwa moto ulikuwa umemchoma.
5. **Baadhi ya maneno na viambishi mbalimbali katika usemi halisi hubadilika sentensi inapoandikwa katika usemi wa taarifa.**

a. **'leo' huwa 'siku hiyo'**

**-'sasa' ikawa 'wakati huo'**

Mfano;

**Usemi halisi:** "Nitawatembelea wangu **leo,**" alisema Grace.

**Usemi wa taarifa:** Grace alisema kuwa/kwamba angewatembelea wanawe **siku hyo.**

b. **'kesho/wiki ijayo/mwaka ujao' huwa 'siku ambayo ingefuata/wiki ambayo ingefuata/mwaka ambao ungefuata'** Mfano:

**Usemi halisi:** "mikate yenu italetwa **kesho,**" alisema Kemei.

**Usemi wa taarifa:** Kemei alisema kuwa mikate yetu/yao ingeletwa **siku ambayo ingefuata.**

**AU**

Kemei alituahidi kwamba mikate yetu ingeletwa **siku ambayo ingefuata**.

c. **Kiambishi "ta" cha wakati ujao huwa "nge".** Mfano;

**Usemi halisi:**"Walimu wa Kiswahili wa**ta**jifunza mengi katika warsha ya Mumias," Riziki alisema.

**Usemi wa taarifa:** Riziki alisema kwamba walimu wa Kiswahili wa**nge**jifunza mengi katika warsha ya Mumias.

d. **Hali timilifu hubadilikuwa wakati uliopita hali timilifu.** Kwa mfano:

**Usemi halisi:** "Wauguzi wa**me**subiri nyongeza ya mishahara yao kwa muda mrefu," akalalamika Profesa Olung'a.

**Usemi wa taarifa:** Profesa Olung'a alilalamika kuwa wauguzi **walibkuwa wamesubiri** nyongeza ya mishahara yao kwa muda mrefu.

e. **Hali ya mazoea hubadilika na kuwa wakati uliopita hali ya mazoea.** Kwa mfano;

**Usemi halisi:** "Wachezaji wa mchezo wa raga **hufanya** hufanya mazoezi kila joni," Tero alimwambia mwandishi wa habari.

**Usemi wa taarifa:** Tero alimwambia mwandishi wa habari kuwa wachezaji wa mchezo wa raga **walikuwa wakifanya** mazoezi kila jioni.

f. **Jana/juma lililopita/mwezi jana** hubadilika na kuwa **siku iliyotangulia/juma lililotangulia/mwezi uliotangulia.** Kwa mfano;

**Usemi halisi:** Likizo fupi ya muhula huu ilikuwa **mwezi jana,"** Vilembwaalisema.

**Usemi wa taarifa:** Vilembwa alisema kuwa/kwamba likizo fupi ya muhula huo ilikuwa **mwezi uliotangulia.**

g. **Viashiria vya karibu pia hubadilika na kuwa vya mbali.** Kwa mfano;

**Hapa** huwa **pale/hapo**
**Huyu** huwa **huyo/yule**
**Hivi** huwa **hivyo/vile**

**Usemi halisi:** "Tutaunda uwanja mwingine wa kuchezea hapa," akatamka Maurice.

**Usemi wa taarifa:** Maurice alisema kuwa wangeunda uwanja mwingine wa kuchea **pale/hapo.**

**Usemi halisi:** "panya ameingia **humu,**" mtoto alimwambia mamake.

**Usemi wa taarifa:** Mtoto alimwambia mamake kuwa panya alikuwa ameingia **humo/mle.**

h. **Viwakilishi vya nafsi za kwanza na pili hubadilika na kuwa vya nafsi ya tatu.** Mfano;

**Usemi halisi: "Ni**takuarifu kesho," Halima alisema.

**Usemi wa taarifa:** Halima alisema kuwa **a**ngemwarifu siko ambayo ingefuata.

**Usemi halisi:** "**U**tahudhuria mkutano wa leo jioni?" Shiyundi alimuuliza Wairimu.

**Usemi wa taarifa:** Shiyundi alimuuzia Wairimu kama **a**ngehudhuria mkutano wa siku hiyo jioni.